Afya ya Akili Kimataifa
Ombi la Mapendekezo ya mradi

Grand Challenge ya Afya ya Akili Kimataifa: Afya ya akili na ustawi wa vijana, Hatua ya 1

Mei 2020

Zingatia: Maombi yatapokelewa kwa Kiingereza na Kifaransa TU

TATIZO

Afya duni ya akili ni tishio kubwa kwa haki za wananchi maskini na walio kwenye mazingira magumu duniani. Mikakati ya kubaini na kutibu changamoto za afya ya akili ambayo ina mafanikio kwenye nchi za kipato cha juu mara nyingi haifai, haisaidii, na inahusisha rasilimali nyingi sana ili kufanikiwa kwenye nchi za kipato cha chini na cha kati na kwa watu walio kwenye mazingira magumu. COVID-19 imezifunua changamoto hizi waziwazi, na kuchochea hitaji la usadizi unaofikika wa afya ya akili huku watu duniani kote wakikabiliana na viwango vipya vya mfadhaiko, wasiwasi, na upotevu. Kwa vijana, jambo hili linaongezeka zaidi. Mzigo mkubwa zaidi wa afya duni ya akili unatokea pale vijana wanapoanzisha nyenzo za kijamii, kitamaduni, kihisia, kielimu, na kiuchumi ambazo kwazo watazitegemea ili kudumisha afya na ustawi kwa maisha yao yote. **Asilimia 75 ya matatizo ya afya ya akili yanaanza kabla ya miaka 24**[1] na kila mara utafiti unaonesha kwamba afya duni ya akili kwa vijana inazorotesha afya, elimu, kipato, na uundwaji wa mahusiano na jumuiya zenye tija. Vijana wanapitia aina nyingi zaidi ya unyanyasaji wa kijinsia ambao unaweza kuwaathiri sana na vibaya wasichana pamoja na wavulana lakini hasa unaweza kuzuia uwezo wa wasichana kuchagua njia yao binafsi. Kujiua kwa sasa ndiyo sababu inayoongoza kwa vifo miongoni mwa vijana wa kike, na, baada ya kubalehe, wasichana na wanawake wana uwezekano mara mbili kukutwa na ugonjwa wa kushuka moyo sana.[2] Ongezeko la visababishi vya mfadhaiko ambavyo gonjwa tandavu la COVID-19 linaweka katika afya ya akili ya vijana unatoa ushahidi zaidi kwa ajili ya kuongeza uwekezaji na uvumbuzi katika eneo hili nyeti lililosahauliwa.

MPANGO WA AFYA YA AKILI KIMATAIFA

Lengo kuu la Grand Challenge ya Afya ya Akili Kimataifa Afya ya akili na ustawi wa vijana itatoa udhamini kwa mawazo ya kijasiri ili kukidhi mahitaji ya kiakili ya vijana wengi walio kwenye mazingira magumu wenye umri wa miaka 10 mpaka 24.

Lengo la **Ombi hili la Mapendekezo ya Mradi (RFP)** ni kuunga mkono **Mawazo ya Kijasiri yenye Matokeo Chanya®** kwa **mbinu za kivumbuzi ili kuboresha ufahamu wa afya ya akili na/au kutoa huduma zilizo rafiki kwa vijana huku zikieleza mambo tata ya kijamii na kimazingira yanayochangia afya ya akili na ustawi wa vijana.** Mbinu hizo zinapaswa kuzingatia utamaduni, na kuendeshwa na jumuiya.

Mapendekezo yote yanapaswa kuonesha ushahidi wa uhusishwaji wenye tija wa vijana wanaoishi maisha husika katika kubuni, kujaribu na utathmini wa uvumbuzi husika

[1] Kessler, Ronald C. et al. Lifetime Prevalence and Age-of-Onset Distributions of DSM-IV Disorders in the National Comorbidity Survey Replication, *Arch Gen Psychiatry*. 2005; 62:593-602
[2] Shirika la Afya Duniani. *Gender Disparities in Mental Health*. Zinapatikana katika: https://www.who.int/mental_health/media/en/242.pdf?ua=1

MAENEO YA KUZINGATIA

Grand Challenges Canada inatafuta mawazo ya kijasiri yaliyobuniwa ili kutekelezwa kwenye nchi zenye kipato cha chini na cha kati, ambayo yanaweka mkazo katika **kuboresha ufahamu wa afya ya akili na/au kutoa huduma zilizo rafiki kwa vijana.** Mawazo haya ya kijasiri yanaweza kubuniwa na mashirika yasiyo ya kupata faida na mashirika ya kupata faida, pamoja na taasisi nyingine zinazotambulika.

Vumbuzi zinazopendekezwa zinapaswa kuwa za kijasiri, za kibunifu, kimageuzi na zinazofikika kwa vijana wengi walio kwenye mazingira magumu, na zinapaswa kuwa na uwezekano wa kuwa endelevu kwa kiwango kikubwa. Vumbuzi zinapaswa kufanya moja au zaidi ya yafuatayo:

1. Kuunga mkono mazingira ya jumuiya yanayoendeleza ustawi wa akili katika kipindi chote cha ujana
2. Kuwasilisha kibunifu ufahamu wa afya ya akili na elimu ya saikolojia ya kijamii, ikifanya kazi ya kujumuisha uelewa wa afya ya akili kwenye jumuiya pana zaidi
3. Kutoa huduma ya uangalizi na urejeshaji iliyo fanisi na nafuu, na iliyo rafiki kwa vijana na inayotekelezwa kijumuiya
4. Kukuza utulivu wa akili na kuchapuza uzuiaji wa matatizo ta akili na uendelezaji wa afya ya akili
5. Kuunganisha huduma za afya ya akili na/au afua za ustawi kwenye mifumo iliyopo ya elimu
6. Kushughulikia mahitaji ya afya ya akili ya vijana waliofanyiwa ukatili kwa mbinu ya kufahamisha vizuri kuhusu kiwewe.
7. Kutumia kibunifu teknolojia inayotumiwa sana na kuaminiwa sana na vijana

UFADHILI ULIOPO

Miradi itakayofanikiwa itapewa ruzuku ya mitaji hadi kufikia Dola za Canada $250,000 kwa kipindi cha miezi 18 mpaka 24 ili kuandaa na kufanya majaribio ya uvumbuzi uliopendekezwa. Takribani misaada ya mitaji 15 itatolewa katika hatua hii.
Vigezo vya Sifa
Mawazo haya ya kijasiri yanaweza kuanzia Canada, Uingereza au nchi za kipato cha chini na cha kati zenye ustahili wa ODA. Shughuli zote za utekelezaji zinapaswa kufanyika kwenye nchi za kipato cha chini na cha kati zenye ustahili. Tafadhali pitia Vigezo vya Kufuzu katika Ombi kamili la Mapendekezo ya Miradi. Waombaji wenye sifa wanajumuisha mashirika ya kijamii na taasisi nyingine zinazotambulika zilizoanzishwa na kusajiliwa kisheria, ambazo zinaweza kutekeleza kwa mafanikio shughuli husika kwenye eneo lao husika la kiufundi, na ambazo zinaweza kupokea na kusimamia fedha za msaada. Kampuni za watu binafsi hazina sifa ya kudhaminiwa. Mashirika ya Kiserikali na ofisi za nchi za Umoja wa Mataifa hazina sifa ya kutuma maombi.

MAELEKEZO YA MAOMBI

Maombi yatapokelewa kwa Kiingereza na Kifaransa TU, na Ombi kamili la Mapendekezo ya Mradi linapatikana kwa Kiingereza na Kifaransa tu. Tafadhali pitia Ombi kamili la Mapendekezo ya Mradi kabla ya kutuma maombi ili kuhakikisha unakidhi vigezo vya kufuzu.

MUDA WA MWISHO WA MAOMBI: Julai 17, 2020 saa 3:00 P.M. ET

Kutokana na muda wa uchakataji, tunapandekeza kusajili akaunti kwenye Fluxx Portal si zaidi ya Julai 9, 2020.

Ili kuomba ufadhili wa fedha, waombaji WANAPASWA kutumia fomu ya maombi ya mtandaoni, inayopatikana kupitia Fluxx Portal ya Grand Challenges Canada (gcc.fluxx.io) kwa Kiingereza na Kifaransa TU.

RASIMU